# LEARNING BY EAR

## "Mihadarati na vileo-poromoko la jamii"

## Episode 4: "Ukweli mtupu"

**Author: Chrispin Mwakideu**

**Editor: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo**

**Proofreader: Charlotte Collins**

**List of characters by scene:**

**SCENE ONE: AT THE POLICE STATION**

- **Beri (f, 45)**
- **Jabali (m,18)**

**SCENE TWO: OKOSHO AND ZULA AT BAMJU'S PLACE**

- **Okosho (m, 18)**
- **Zula (m, 18)**
- **Bamju (m, 40)**

**SCENE THREE: INSIDE THE SCHOOL HALL AT LIMBI HIGH**

- **Bi. Chacha (f, 45)**
- **Chambo (m, 30)**
- **5-6 Mixed voices (m/f, 14-18)**

**MSIMULIZI (m/f)**

**<u>INTRO:</u>**

Hujambo na karibu tena katika kipindi cha Noa bongo! Jenga maisha yako, tukiendelea na hadithi hii kuhusu madhara ya matumizi ya mihadarati na vileo, kwa jina **“Poromoko la jamii”.** Tuliachia kipindi kilichopita wakati Kamishna Beri alikuwa akimhoji mshukiwa mmoja aliyekamatwa na Inspekta Tino. Kule mjini, Puyanga, mumewe Beri alikutana na Bamju kumfahimisha kuhusu mihadarati iliyotarajiwa bandarini ambayo ingehitaji wauzaji wengi. Je Bamju atafanikiwa kupata wauzaji hao? Ni kina nani atakaolenga kwa biashara hii? Kumbuka Chambo, mwanzilishi wa “Youth watch” amepanga mjadala na wanafunzi wa shule ya upili ya Limbi kuhusu ubadirifu wa mihadarati na vileo. Moja kwa moja tupate kipindi cha leo, kiitwacho **“Ukweli mtupu”**. Tunaanzia pale Jabali akibumburuka kwenye kituo cha polisi- akiwa na maruwe ruwe ya usiku uliopita.

**SCENE ONE: AT THE POLICE STATION**

1. **JABALI:** **(awakening)** Arrgh! Hapa ni wapi jameni?

2. **BERI:** Sisi ndio tunaouliza maswali mahali hapa, kijana. Unaitwa nani? Ulikunywa nini jana usiku? Tulikupata nusu uchi nje ya kilabu 2000. Ulikuwa umejikojolea na kujitapikia kila mahali. Unajuwa ni makosa kufanya hivyo hadharani.

3. **JABALI:** **(starts to remember)** Mungu wangu… hapana! Kwani walinipa nini? Fyuu - ninanuka… mimi... tafadhali nisameheeni. Hiyo ilikua mara yangu ya kwanza, na…

4. **BERI:** Bila shaka. Sikiliza – nitakuachilia mara hii, kwa sababu unaonekana kijana mzuri aliyejichanganya na vijana wabaya. Lakini nikikuona tena hapa, itakua kesi ingine. Umenielewa?

5. **JABALI:** Ndio. Asante, je naweza kupata maji na dawa za maumivu?

6. **BERI:** **(firmly)** Kijana hapa si hospitali – hiki ni kituo cha polisi. Hebu shika njia kabla sijabadilisha mawazo.

7. **SFX: FOOTSTEPS QUICKLY LEAVING**

8. **SFX: BERI SITS DOWN ON A CREAKING CHAIR AND HITS ON HER DESK**

9. **BERI:** **( to herself)** Ah Puyanga, mumewangu... itanibidi nikuchukulie hatua kama afisa wa polisi na sio kama mkeo. Haya yamezidi unga sasa. Maisha ya vijana wadogo yanaharibika.

10. **MSIMULIZI:**Beri anasema ukweli.tatizo la mihadarati limekuwa sugu sehemu nyingi, sio hapa tu. Vijana wasio idadi wanaathirika na kupoteza maisha yao. Wakati Jabali akitoweka kutoka kituo cha polisi, Bamju alikua amejipatia wauzaji wawili wa mihadarati. Hujakosea: ni marafiki wa Jabali, Okosho na Zula. Wote wa tatu walikua wameketi nyumbani kwa Bamju wakipanga utenda kazi wao.

**<u>SCENE TWO: OKOSHO AND ZULA AT BAMJU'S PLACE</u>**

11. **BAMJU:** Sawa, mpango ndio huu. Unahukua mali, unauza, unaleta pesa na ninakulipa papo hapo. Sitaki ujanja. Nikikutaka ninajuwa pakukupata!

12. **ZULA:** **(excited)** Lo! Poa mamen. Ni kama kwenye filamu, si unajuwa, mafioso na magenge yao

13. **OKOSHO:** Fyata mdomo wako, Zula. Acha mzaha hii ni kazi. Sawa, sasa tunawauzia kina nani ? Na je tukishikwa? Utatusaidia?

**14. BAMJU:** Hujui wanunuzi wenu ni kina nani? Si wengine bali ni vijana: marafiki zenu, watu kwenye maeneo ya shule. Unafikiria mimi ni mjinga kuwaajiri? Bila shaka, nitaajiri wengine baadae, watu ambao ni vigumu kushukukiwa – waombaji mitaani, wapiga rangi viatu, wauzaji magazeti. Kazi yenu nikuuzia wanafunzi. Sheria ni moja tu katika hii kazi! Usikamatwe!

**15. ZULA:** **( very excited**) Nilikwambia, Okosho, hii ni kama tuko kwenye bonge la picha!

**16. BAMJU:** Rafiki yako anaota kuwa yeye ni muigizaji wa filamu? Shika. Sehemu yako ya madawa ndio hii.

**17. OKOSHO:** Huwezi kutueleza haya madawa ya kulevya ni gani? Itakuwa vigumu kuuza tusichokijuwa.

**18. ZULA:** Kweli – au kitu ambacho hatujatumia.

***19.* BAMJU:** Sina hakika mimi mwenyewe lakini nashuku ni ***brown sugar.***

**20. ZULA:** Sugar? Wacheni matani? Yani tunakwenda kuuza sukari?

***21.* OKOSHO:** Wewe pumbavu! Hilo ni jina lengine la ***heroine.***

**22. ZULA:** Ei! jamani! ….Hii sinema kali sana.

**23. MSIMULIZI:** Ubaya wa hii mihadarati ni kule kuwapatia watu utajiri wa haraka, lakini ni maisha yaliojawa na usaliti, njama, na hofu kuu ya kutiwa mbaroni na kufungwa. Haya ndiyo maisha Okosho na Zula waliojiingiza. Kwa sasa, tujiunge na wanafunzi wa Limbi waliokuja kumsikiliza mzungumzaji Chambo akinasihi kuhusu athari za mihadarati na vileo vyengine – na yupo mwanafunzi fulani wa kale pia kwenye hadhira.

**SCENE THREE: INSIDE THE SCHOOL HALL AT LIMBI HIGH**

**24. SFX: HIGH SCHOOL AMBIENCE**

**25. SFX: Ringing bell**

**26. BI. CHACHA:** Asanteni, tuwe na mkutano mmoja tafadhali! Leo tumekirimiwa kuwa na mgeni katika shule yetu. Bw. Chambo ambae ni mwanzilishi wa shirika la Youth Watch, shirika lisilo la kiserikali linalohamasisha vijana kuepuka mihadarati maishani mwao. Tumkaribisheni pamoja!

**27. SFX: APPLAUSE FROM STUDENTS**

**28. BI. CHACHA:** Asanteni, asanteni sana. Sasa, bila ya kuganzaganza, nitamuachia usukani Bw. Chambo. Tafadhali endelea.

**29. CHAMBO:** **(firmly)** Kwanza kabisa napenda kuweka wazi kuwa sikuja hapa kuwatishia, kuwatumbuiza au kuwaboesha.

**30. SFX: MURMURS AND GIGGLES FROM STUDENT CROWD**

**31. CHAMBO:** Niko hapa na azma ya kuajulisha athari za mihadarati na vileo vyengine. Sio kwamba nalipwa kufanya hivi, lakini ni kwa sababu mimi ni manusura wa mihadarati, na nisingelipenda kumuona yeyote kati yenu akiangamizwa na mihadarati hiyo. Kwa kuanza, acheni niwasomee mada zilizogonga vichwa vya habari katika magazeti yeti nchini.

**32. SFX: NEWSPAPERS BEING SHUFFLED AND PAGES OPENED (studio)**

**33. CHAMBO: (starts to read)** Idadi ya watumizi wa madawa ya kulevya yaongezeka Chunga Sana. Ulevi unakisiwa kuwa sababu ya nyumba nyingi kuvunjika. Kitengo cha afya ya jamii kinakumbwa na uzito wa kutibu maradhi yanayosababishwa na athari ya uvutaji wa tumbaku.

**34. SFX: NEWSPAPERS CLOSED (studio)**

**35. CHAMBO:** Naweza kumaliza muda wote nikisoma tu vichwa hivyo vya habari...

**36. BI. CHACHA:** Inashtusha mno. Labda ungeliwaeleza wanafunzi haswa, madawa au mihadarati ni nini?

**37. CHAMBO:** Swali zuri. Madawa ni kemikali yeyote inayoleta ubadilifu wa mwili, akili, hisia au hata tabia. Mihadarati kwa hivyo ni utumizi mbaya wa madawa au kemikali halali au haramu, yatakayo sababisha uharibifu wa mwili, hisia, akili, au tabia.

**38. BI. CHACHA:** Umesema utumizi mbaya wa madawa halali au haramu. Kwa hivyo mtu anaweza kutumia vibaya tembe, au dawa nyengine zinazopatikana madukani au hata zile alizopewa na daktari? Tuseme, kama, tembe za malaria?

**39. SFX: HUGE LAUGHTER FROM STUDENT CROWD**

**40. CHAMBO:** Utumizi mbaya ni utumizi mbaya. Naamanisha, ndiyo, unaweza kutumia vibaya dawa ulizoagizwa na daktari. Tayari nimewafafanulia maana ya dawa, na mwili wako unapokuwa unategemea dawa hizo, basi unakuwa muathirika.

**41. BI. CHACHA:** Bw. Chambo, je, ni wavulana pekee wanaoathirika na mihadarati? Muda mwingi hapa shuleni kwangu nimepata ripoti za wavulana kwa wingi kuliko wasichana … hmmm. Wengine wao walimaliza mithani yao mwaka jana.. walitoa moshi kama gari-moshi!

**42. SFX: SCATTERED CHEERS AND CLAPS FROM GIRLS**

**43. CHAMBO:** Ni kweli muda mwingi wavulana hupenda kufanya utafiti zaidi kuliko wasichana. Lakini haimaanishi wasichana hawaathiriki. Kinyume chake, takwimu zinaonyesha kuwa idadi kubwa ya wanawake inatumia pombe na madawa ya kulevya tena kuanzia umri mdogo. Wangapi wenu wanajua watu walioathirika? Inaweza kuwa sigara, pombe, miraa, bangi, heroini, unga, aspirini, gamu ya viatu - hata chai na kahawa inayo kemikali inayolevya.

**44. SFX: MURMURS AND MUMBLES AGAIN FROM STUDENTS**

**45. CHAMBO:** Kote ninapouliza swali hili, jibu ni moja. Aghlabu mikono yote huinuliwa. Aila yangu ilibidi inifukuze - Siyo kwa sababu hawanipendi, bali athari ya madawa ilinizidi nikaanza kuiba vitu nyumbani ili kukimu hamu ya mihadarati hiyo.

**46. BI. CHACHA:** **(sadly)** Kijana wangu yuko hali hiyo. Hakuna afanyalo ila kuvuta tumbaku na kutafuna mairungi usiku na mchana. Kuna siku aliniambia machoni pangu kuwa iwapo sitampa pesa za kununua mairungi basi ataniua.

**47. CHAMBO:** Kijana wako, mwalimu, anahitaji msaada – kama nilivyohitaji, na kama wengine walionaswa na mihadarati. Najuwa wengi wenu mumeanza kutumia mihadarati na vileo. Nawaomba muachane nayo kungali mapema kabla hayajawateka nyara. Iwapo hujui utafanyaje, tafadhali nione baada ya maongezi haya.

**48. BI. CHACHA:** Bw. Chambo, kabla tumalize, tafadhali tueleze: utajuwaje kama mwanafunzi, au kijana, bwana, kaka, dada, au ndugu katika familia anatumia mihadarati? Ishara ni zipi? Kwa sababu kijana wangu alinishangaza!

**49. CHAMBO:** Zipo ishara, lakini haitoshi kujiamulia bila kuwa na uhakika. Kwa mfano, Unaweza kuona macho yake yameiva damu au mekundu mno, mabidiliko katika hamu yake ya kula au kulala kwake pamoja na kupunguka au kuongezeka kwa uzito wa mwili, pia kiharufu katika pumzi zake, mwili au nguo kwa ajili ya uchafu wake.

**50. BI. CHACHA:** Ah, kumbe ndio kwa maana kijana wangu amekondeana vile - hamu ya chakula imemwisha sio kama awali. Zipo ishara zingine?

**51. CHAMBO:** Ndio, nyengine ni tabia za waathiriwa wa mihadarati, hususan wanafunzi shuleni, kutoroka shuleni au kuzoroteka kimasomo, pia wanageuza marafiki na kuanza kwenda nje usiku au kubadili michezo, lakini kubwa zaidi ni uhitaji mkubwa wa pesa bila kujulikana anazitakia nini, au matatizo ya kifedha. Hili huwalazimu kukopa au kuiba.

**52. BI. CHACHA:** Shukran, Bw. Chambo. Yamkini kuna mambo mengi twawezakujifunza kuhusu mihadarati, twaomba tukualike tena baada ya majuma mawili, ili wanafunzi nao wapate fursa ya kukuuliza maswali. Hebu tumpongezeni Bw. Chambo wa shirika la Youth Watch.

**53. SFX: WILD APPLAUSE AND CHEERS FROM STUDENT CROWD**

**OUTRO:**

Wakati wanafunzi wa Limbi wakimpigia makofi Chambo, Kule nyuma mikono miwili ilikuwa imebanwa, kwani mwenyewe alikua yuatetema kwa yale aliosikia. Hii ilikua mikono ya Jabali. Je ni wasiwasi tu, au bado ana cheche za ulevi? Atafanya nini baada ya hapa? Mihadarati ikishushwa bandarini kwa wingi, Chambo atashinda vita hivi kweli? Na je Beri? Atakua na ujasiri wa kumtia mbaroni mumeo? Kumbuka aligundua madawa kwenye droo. Usikose kujiunga nasi tena ili ujue yote. Ukipenda kusikiliza tena kipindi hiki tembelea tovuti zetu www.dw.de/lbe. Hadi wakati mwengine - kwaheri.